BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 07 Mei, 2025**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 01 Machi, 2025.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2025/2026.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa Mwaka 2025/2026.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

9. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

   Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mapenzi makubwa iliipatia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar shamba liliyopo Bagamoyo eneo la Makurunge ambalo lilikuwa linatumika kwa ufugaji Zanzibar.

   (a) Je, ni ipi hatma ya shamba hili hadi sasa kwa Serikali yetu ya Zanzibar.

   (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuliendeleza shamba hili ili iweze kujiongezea mapato.

   (c) Je, Serikali haioni kuendelea kuliacha shamba hilo bila ya uwekezaji ni kujiingizia hasara hasa huku ikiendelea kuwalipa wafanyakazi walioko huko.

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

92. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

    Je, tathmini iko vipi juu ya mifumo ya usimamizi wa rasilimali watu Serikalini.

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

266. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

     Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu ya mikopo kwa vijana na watu wenye mahitaji maalum.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

59. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Ofisi za Wakala wa Matukio ya Kijamii ni moja kati ya taasisi muhimu katika nchi yetu na wananchi wanapata huduma zao kwenye maeneo haya.

    Je, ni lini Serikali itajenga majengo ya kutosha katika maeneo yenye upungufu wa Ofisi za Wakala wa Matukio ya Kijamii hapa Zanzibar.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

1. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

    Ni lini Serikali itaondoa kipengele cha kununua magari ya taasisi za Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

6. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

    Yanayojitokeza katika usimamizi wa miradi mingi ya Serikali inayoendelea Zanzibar, inaonesha dhahiri kwamba majukumu yaliyokabidhiwa kisheria kwa Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) hayaendani na uwezo wake.

    (a) Je, kwa miaka minne iliyopita (2020 - 2024), ni miradi mingapi ya majengo ya Serikali iliyopaswa kusimamiwa na ZBA kama Mshauri Elekezi na haikuisimamia.

    (b) Je, katika ulimwengu huu wa ushindani, Serikali itaifanyia lini mapitio Sheria inayohusiana na ZBA ili kuinasua Taasisi hiyo kutekeleza majukumu isiyo na uwezo nayo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

272. MHESHIMIWA SALMA MUSSA BILAL (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kiasi gani skuli za watu binafsi zinatoa mashirikiano ya mabadiliko ya utekelezaji wa mtaala mpya wa umahiri.

**Wizara ya Afya:**

100. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Je, tathmini ya ugonjwa wa figo iko vipi kwa sasa.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

37. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Michezo ya kuogelea na mbio za marathoni (marathon) ni miongoni mwa michezo ambayo imekuwa ikitoa heshima kubwa kwa baadhi ya mataifa yakiwemo ya Kenya na Ethiopia. Kwa kiasi kikubwa uwekezaji katika michezo hii umesahaulika hapa Zanzibar.

(a) Je, Serikali haioni kuna haja ya kuihamasisha michezo hii ili iweze kuibua vipaji vya vijana.

(b) Je, ni ipi tathmini ya ushiriki wa vijana katika michezo ya kuogelea na mbio za marathoni (marathon) kwa Zanzibar.

(c) Je, Serikali hupanga bajeti ya kiasi gani katika kuhamasisha michezo hii hapa Zanzibar kwa kila mwaka.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

11. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Katika nchi yetu yapo maeneo mbali mbali yanayochimbwa mawe, kifusi na kokoto ikiwa ni pamoja na eneo la Pujini,

ambapo wananchi katika maeneo haya wanapata usumbufu mkubwa wa kuvamiwa na mavumbi ndani ya vijiji vyao, jambo ambalo linaathiri afya za wananchi hao.

(a) Je, kwa kiasi gani Serikali inalitambua jambo hili.

(b) Je, ni lini Serikali itawaondolea wananchi wa Pujini kadhia hii.

(c) Je, ni lini Serikali itafikiria namna bora ya kuwapatia fidia wananchi wa Pujini kwa usumbufu huo wanaoupata.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

98. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Tathmini iko vipi juu ya ongezeko la usajili wa biashara kwa wawekezaji wanaotokana na sekta ya utalii.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2025/2026.

Zanzibar, (Raya Issa Msellem)
07 Mei, 2025. KATIBU WA BARAZA